

Huduma pepe (virtual) katika NSW



Virtual care in NSW

Swahili

Huduma pepe ni nini?

Huduma pepe (Virtual care), ambayo wakati mwingine inaitwa huduma pepe ya afya (telehealth), inaeleza njia nyingi unazoweza kupata huduma ambayo hazitoi ana kwa ana. Hii ni pamoja na:



mikutano ya video mtandaoni



simu



kutumia vifaa kufuatilia na kusimamia afya yako nyumbani.

Labda umeshawahi kuitumia, kama vile kupata agizo la kurudia kutoka GP wako au kuzungumza matokeo ya kipimo. Mifano mingine inajumuisha ukarabati wa mtandaoni na kutumia vifaa kufuatilia afya yako huko nyumbani.

Huduma pepe haichukui nafasi ya utunzaji wa uso kwa uso, bali inaongeza. Bado utakuwa na uchaguzi kupata huduma halisi wakati inaofaa kwako.

Wewe na daktari wako mnaweza kuamua pamoja kama huduma pepe inafaa kwako.

Je, ni faida gani za huduma pepe?

Huduma pepe hukupa chaguo zaidi za jinsi ya kupata huduma ya afya. Pia linaweza kurahisisha kwako kupokea huduma.

Kuna faida nyingi kupokea huduma yako kwa pepe. Unaweza:

- kupata huduma nyumbani au karibu nyumbani
- kupunguza muda wa safari na gharama, kukupa muda zaidi wa mambo ambayo ni muhimu kwako
- kujumuisha jamaa wa familia, watunzaji au watoaji wengine wa huduma ya afya katika miadi yako, bila kujali walipo
- kuunganisha na huduma za kitaalam, ikijumuisha wakalimani, ambazo zinaweza kutopatikana katika eneo lako la mtaa. Kwa mfano, ikiwa unakaa mji wa shambani unaweza kuunganishwa na wataalamu katika maeneo ya miji makuu.

Huduma pepe hukuunganisha na huduma sahihi, wakati na mahali unapoihitaji.

Inafanya kazi jinsi gani?

Mikutano ya huduma pepe ni mikutano ya kila mara – tofauti kuu ni unazungumza na daktari wako kwenye simu au kwenye skrini.

Huduma pepe hutumia teknolojia sawa na unayotumia kupiga simu au kupigia video marafiki yako na familia.

Kabla ya mkutano wa huduma pepe, utapewa maelezo kuhusu jinsi ya kuunganisha, ni nini ya kutazamia na jinsi ya kupata msaada.

Wakalimani wanapatikana kwa mikutano ya Huduma pepe. Uliza daktari wako kwa maelezo zaidi.

Ninahitaji vifaa gani?

Kwa mikutano mingi unahitaji tu ufikiaji wa simu, au kompyuta, kompyuta kibao au iPad na muunganisho wa mtandao unaotegemewa.


Iwapo huna ufikaji kwa vifaa hivi unaweza kuuliza daktari wako kuhusu njia badala kujiunga mkutano.

Vifaa vyovyote maalam kama vile vifaa vya kufuatilia vitatolewa kwako.

Mikutano mingine ya huduma pepe itatumia baadhi ya data zako za mtandao. Kwa mfano, simu ya video ya dakika 15 itatumia takriban 80MB ya data zako. Matumizi ya data inategemea mipangilio yako ya simu binafsi ya mkononi au mtandao wa nyumbani.

Huduma pepe ni salama na ya faragha?

Ndiyo. Huduma pepe ina viwango sawa vya salama na ufaragha kama huduma ya ana kwa ana. Mifumo tunayotumia katika NSW Health imepimwa kuhakikisha iko salama na udhibiti.



“Huduma pepe ina maana mtoto wangu anaweza kupata utunzaji nyumbani”

Habari zaidi

Tembelea tovuti ya NSW Health ili kujua zaidi kuhusu huduma pepe:
www.health.nsw.gov.au/virtualcare

Kupata usaidizi wa lugha piga simu kwa Huduma ya Utafsiri na Ukalimani: 131 450

